SHULE YA SEKONDARI IHANGO,
S.L.P 6599,
**MBEYA.**
02/12/2020

KUMB NA IHSS/JOIN/2018

NDUGU_______________________________
S.L.P___________
**MBEYA.**

YAH: **MAELEKEZO/MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IHANGO ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA MKOA WA MBEYA KWA MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari kidato cha kwanza katika shule hii ya Sekondari Ihango kwa elimu ya sekondari ili kuanza kidato cha kwanza mwaka 2021

**1.2 SHULE ILIPO NA MUDA WA KURIPOTI SHULENI**

Shule ya Sekondari Ihango ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Mkoa wa Mbeya. Shule ipo umbali wa KM 16 kutoka Mbeya Mjini na KM 3.4 na kutoka karibu na msitu wa Kawetere na barabara ya kuelekea Chunya Mjini.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021 yaani ni ndani ya siku saba uwe umeripoti shuleni

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**2.1.1 WASICAHANA**

- Shati 2 nyeupe za mikono mifupi
- Sket imbili-moja ya khaki na ingine ya rangi ya damu ya mzee, ziwe ndefu sentimeta 5-10 kutoka miguuni, yenye marinda yasiyopungua kumi na sita (16) na yasiyozidi ishirini (20)
- Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino virefu
- Sweta mbili, moja la damu ya mzee na jingine la kijani
- T-shirt nyeupe (babalance) mbili (2) rangi nyeupe
- Soksi nyeupe pea tatu (3)

**2.1.2 WAVULANA**

- Shati 2 nyeupe za mikono mifupi
- Suruali mbili – moja ya khaki na ingine ya rangi ya damu ya mzee, ziwe ndefu kugusa viatu na ziwe na marinda mawili (isiwe modal au flat front)
- Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino virefu
- Sweta mbili, moja la damu ya mzeena jingine la kijani
- T-shirt nyeupe (babalance) mbili (2) rangi nyeupe
- Soksinyeusipea tatu (3)

**KUMBUKA:**Hijabu kwa wasichana ni kitambaa cheupe na hii ni kwa Waislamu tu

**2.2 SARE ZA MICHEZO**

T-shirt ya blue na trackya blue kwa wavulana
T-shirt ya blue na track ya blue kwa wasichana

**2.3 VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

Daftari kubwa **kaunta (Four Quires) ziwe 9 na ndogo ziwe 9,** mkebe mpya, rula, kalamu za wino za kutosha na kalamu za risasi

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

## SHULE YA SEKONDARI IHANGO

## FOMU YA AHADI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi____________________________msichana/mvulana ninakubali kujiunga na kidato cha kwanza hapa Shule ya Sekondari Ihango kama mwanafunzi wa kutwa, leo tarehe__/___/20____. Nitafika shuleni bila kukosa au bila kuchelewa.

Nitatii sheria za shule na nitaishi maisha mazuri na ya mfano. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea, sitakuwa mtoro shuleni.

Sahihi ya Mwanafunzi_________________ Tarehe__/___/20____

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

1. Mimi_______________________________ambaye ni mzazi/mlezi wa mtoto tajwa hapo juu, ninakubali mtoto wangu_____________________________ asome katika Shule ya Sekondari Ihango kuanzia tarehe _____________Ninaamini kuwa ELIMU NI URITHI WA MTOTO na MWANGA WA MAISHA

2. Ninaahidi kumpa/kumtimizia mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo shuleni kama ilivyoagizwa katika barua ya kujiunga na shule yako.

3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu atii sheria zote za shule na kuishi maisha mazuri na ya mfano kwa wenzake. Nitamhimiza asome kwa bidii katika masomo yake na kazi za kujitegemea. Nitamhimiza asiwe mtoro shuleni.

4. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi_____________________

5. Sahihi ya Mzazi/Mlezi___________________ Tarehe__/___/20____

**C. MATUMIZI YA OFISI TU**

Mwanafunzi_____________________________________ amepokelewa hapa shuleni tarehe__________________

Jina la Mwalimu__________________________________

Sahihi_____________________

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**

**MBEYA DISTRICT COUNCIL**

IHANGO SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 6599,
**MBEYA.**
02/12/2020

Ref: IHSS/JOIN/2018

THE MEDICAL OFFICER
________________HOSPITAL
P.O Box
**MBEYA.**

Re: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine______________________________________ as to his/her fitness to pursue further education at this school

1. Hemoglobin_________________________________________________
2. P.V bleeding________________________________________________
3. Blood pressure______________________________________________
4. Blood group_________________________________________________
5. Sight_______________________________________________________
6. Hearing_____________________________________________________
7. Urine for sugar and pregnancy test___________________________
8. Stool for routine examination_______________________________
9. Skin diseases________________________________________________
10. Asthma_____________________________________________________
11. Leprosy____________________________________________________
12. Epilepsy___________________________________________________
13. PulmonaryTuberculosis____________________________________
14. Deformity__________________________________________________
15. Mental problem____________________________________________
16. V.D (give type) ___________________________________________
17. Any other serious diseases not mentioned above

***PLEASE SIR/MADAM, PROVIDE US WITH RELEVANT CONDITIONAL EVIDENCES OF THE NAMED PERSON SO AS TO HELP US IN CASE A STUDENT FACES HEALTH PROBLEMS***

Comments__________________________________________________________________________
_________________________________________________________________________________

Dr/C.O(Full Name)___________________________ Signature______________________

Yours

___________________

# 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

3.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978** kama ilivyorekebishwa kwa **Sheria Na**. **10 ya Mwaka 1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na **Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi** yenye dhamana ya elimu hapa nchini chini ya **Ofisi ya Rais – TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu nchini Tanzania

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni tayari kwa masomo.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(b) Mahudhurio mazuri katika shughuli za nje na ndani ya shule kulingana na ratiba ya shuleni lazima
(c) Kushiriki kwa umakini na kufanya maandalio ya jioni (evening preparation)
(d) Kuwahi katika shughuli za shule na zingine utakazopewa
(e) Kufahamu na kuzingatia mipaka ya shule; kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shuleni na katika shughuli za nje na masomo
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Kutunza mali za umma

**3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA MASOMO**

(a) Wizi
(b) Uasherati
(c) Ubakaji
(d) Kumpiga mwingine,kupigana, kutukana au kutukanana
(e) Kupata mimba/kusababisha mimba
(f) Kutoa mimba
(g) Kugoma, kuchochea mgomo, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(h) Kukataa adhabu kwa makusudi
(i) Kuwa na simu ya mkononi
(j) Kudharau bendera ya taifa
(k) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(l) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bhangi, kokeini, mirungi, kubeli na kadhalika

**4.0 MAMBO MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

Fomu ya daktari (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na MGANGA MKUU wa HOSPITALI YA SERIKALI. Fomu hii iwasilishwe Ofisi ya Mkuu wa Shule mara tu utakaporipoti. **Daktari aeleze matatizo yote ya mtoto ili kuepusha usumbufu akiwa shuleni.**

Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo wowote katika kipindi chote cha uanafunzi wako na makosa mengine ya jinai

Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

NB: Tafadhali soma kwa makini maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu ndani ya muda mwafaka. Maagizo yote kama **sare za shule aina zote na sare za michezo** vikamilishwe bila usumbufu wowote. Mtoto wako hatopokelewa hapa shuleni bila daftari zote zinazohitajika pamoja na sare za shule

***"ELIMU NI HAZINA"***

KARIBU SANA IHANGO SEKONDARI

_________

**MKUU WA SHULE**